# Mtagusano wa Uforensiki na Riwaya ya Kiswahili: Mfano kutoka Riwaya ya 'Mzimu wa Watu wa Kale'

*Neema Julius Luhwago*
*Chuo Kikuu cha Dodoma*

**Ikisiri**

**Makala haya yanahusu mtagusano wa uforensiki katika riwaya ya Kiswahili. Pia, yanaonesha namna taaluma ya uforensiki inavyojitokeza katika riwaya ya Kiswahili na kuonesha mtagusano ambao umejenga maudhui na fani katika riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale* kwa kujikita katika vipengele vya: wahusika, msuko wa matukio, muktadha, matumizi ya lugha, mgogoro na mtindo wa usimulizi wa kiforensiki. Aidha, makala haya yanatambulisha uhusiano uliopo kati ya taaluma ya Uforensiki na Fasihi katika kufikisha ujumbe kwa jamii husika. Makala haya yatatumia nadharia ya mwingiliano matini ambayo itasaidia kuweka bayana namna taaluma ya uforensiki inavyojitokeza katika riwaya ya Kiswahili. Makala haya pia, yataibua tafakuri mpya ya riwaya ya Kiswahili na uforensiki itakayoleta chachu kwa wanataaluma na wahakiki wa kazi za fasihi katika zama hizi za Sayansi na Teknolojia.**

**Maneno Muhimu:** Mtagusano, Forensiki, Teknolojia, Fasihi, Riwaya

## Utangulizi

Riwaya ya Kiswahili imekuwa ikihakikiwa na kutafitiwa na wanataaluma wa fasihi kwa kuibua dhana na mitindo mbalimbali katika fani na maudhui ya riwaya. Dhana kama vile ufutuhi, upelelezi zinginezo zimekuwa zikiibuliwa kwenye kutazama maudhui hususani dhamira kama vile, mapenzi, ujasusi, upelelezi, uhujumu uchumi, uongozi na zinginezo. Katika fani, uhakiki na tafiti nyingi zimekuwa zikiangalia msuko wa matukio, wahusika, madhari na mtindo n.k. Madumulla (2009), anaielezea riwaya ya Kiswahili katika mikondo yake ambayo ni mikondo ya kisafari na kimaadili mfano wa riwaya hizo ni *Uhuru wa Watumwa*, *Kusadikia na Kufikiria*. Mkondo wa kiethnografia una riwaya kama *Bwana Myombekere na Bibi Bugonoka*. Mkondo wa kihalifu na kipelelezi una mifano ya riwaya kama vile *Mzimu wa Watu wa Kale*, *Kosa la Bwana Msa*, *Simu ya Kifo*, *Njama*, *Hofu* na zinginezo. Mkondo wa kijamaa, mkondo wa uhalisia teti, mkondo wa kitafakari na mkondo wa ufungwa. Zaidi ya hayo, anafafanua aina za riwaya ya Kiswahili ambazo ni riwaya ya kitawasifu, riwaya ya kiwasifu,

riwaya ya kimaadili, riwaya ya kihistoria, riwaya ya kielimu, kisaikilojia, kimapinduzi, kifalsafa na riwaya pendwa. Makala haya yanaeleza mtagusano uliopo kati ya uforensiki na riwaya ya Kiswahili ambao unajitokeza katika riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale.* Katika sehemu inayofuata, nimefafanua istilahi muhimu zinazoendana na mtagusano na uforensiki.

### Mtagusano

Kamusi ya Kiswahili Sanifu (2013) toleo la 3, inafasili neno mtagusano kuwa ni hali ya vitu viwili kuingiliana. Katika makala haya tunazungumzia mwingiliano wa uforensiki na fasihi unaojipambanua kupitia riwaya ya Kiswahili.

### Uforensiki

Eckert (1992) ameelezea uforensiki kuwa ni taaluma ihusuyo kumtambua mhalifu kwa njia ya kisayansi kama vile uchunguzi wa alama za vidole na vithibiti halisi kama vile vipimo vya kibiolojia, nywele, udongo na vitu vingine vilivyoachwa katika eneo ambalo uhalifu ulifanyika. Kwa mfano, polisi hutumia vipimo maalum ili kujua kiwango cha kilevi kwa dereva aliyesababisha ajali. Katika hili, Eckert aliandika, "*Alcohol intoxication is one of the most frequent causes of accidents presented*." (Tafsiri yetu) "Mara nyingi, ulevi ni moja kati ya vyanzo vya ajali zinazoripotiwa." Akielezea maendeleo katika sayansi ya uforensiki, Eckert anasema,

> *Modern forensic sciences and their practical applications originated in the middle of the nineteenth century. Previously, because of lack of sophistication in chemistry, physics, biology, and medicine, investigation of trace evidence and suspicious poisoning deaths was largely subjective, which led to great controversy and legal challenges during court trials. Eckert* (1992: 21).
>
> Sayansi ya uforensiki wa kisasa na matumizi yake yalianza katikati ya karne ya 19. Kabla ya hapo, kutokana na uduni katika taaluma za kemia, fizikia, biolojia na tiba, uchunguzi wa ushahidi ashiria na mahisio ya vifo vinavyosababishwa na sumu villikuwa tegemezi, hali iliyopelekea changamoto za kisheria katika utoaji wa hukumu mahakamani. (Tafsiri yangu)

Naye Bondergaard (2017) anaeleza kuwa neno uforensiki limetokana na neno la kilatini "*forensis*" lenye maana ya "f*orum*" lenye maana ya jukwaa la kujielezea. Hivyo, ni ujuzi wa kuzungumza katika mihadhara ya kisiasa au mahakama. Anaendelea kusema kwamba matumizi ya uforensiki yanajibainisha zaidi katika mahojiano ya kimahakama yanayohusiana na maarifa ya kisayansi yanayodadavua viashiria vya matendo ya kihalifu na kuleta ushahidi. Jambo tunaloliona hapo ni uhusishwaji wa matumizi ya lugha na sayansi katika ufafanuzi wa uthibitisho wa matendo ya kihalifu yanayotakiwa kutolewa

hukumu. Matumizi hayo ya mahojiano ndiyo yaliyosababisha kutokea kwa uforensiki katika lugha.

Kwa mantiki hiyo, tunaona jinsi ambavyo taaluma ya uforensiki inavyojitokeza katika lugha na kuweza kutumika katika uchunguzi wa uhalifu utokanao na lugha ya mazungumzo au maandishi. Fasihi andishi hujipambanua katika tanzu kuu tatu ambazo ni ushairi, riwaya na tamthiliya. Katika makala haya tunajikita katika riwaya hususan ya Kiswahili na kuchunguza mtagusano wa uforensiki katika riwaya teula za Mohamed Said Abdula ambazo ni Mzimu wa Watu wa Kale na Kosa la Bwana Msa. Uchaguzi wa riwaya hizi umetokana na kwamba ni miongoni mwa riwaya zinazojipambanua katika mkondo wa kihalifu (Madumulla, 2009) kutokana na maudhui yake ya ujasusi, ujambazi, upelelezi n.k.

Malcolm (2017) anaeleza kuwa hivi karibuni uforensiki umeanza kujitokeza kwenye sarufi ya lugha katika kutambua, kubainisha, kuainisha na kutathmini uhalisi wa jambo kwa kutumia mbinu za kisayansi na teknolojia ili kupata ushahidi thabiti kuhusu jambo fulani katika jamii. Malcolm na wenzake (2017:14) wameandika kuwa:

> "*Forensic linguistics is a sub-field of linguistics that is particularly engaged with professional and institutional interaction in legal context. At the heart of linguistics are the basic building blocks of language, its sounds, words, grammar, meanings and functions: phonetics, phonology, lexis, syntax, semantics, and pragmatics, which we use to describe what we see"*
>
> Isimu forensiki ni tawi mojawapo la isimu linaloshughulikia mtagusano wa kitaaluma na kitaasisi katika muktadha wa kisheria. Msingi wa isimu umejengwa na viamba jengo vya lugha ambavyo ni sauti, maneno, sarufi, maana na matumizi: fonetiki, fonolojia, leksika, sintaksia, semantiki na pragmatiki, ambavyo tunavitumia kuelezea kile tunacho kiona." (Tafsiri yetu).

Katika isimu, uforensiki unajitokeza zaidi katika uchunguzi wa uhalifu utokanao na lugha ya mazungumzo au maandishi, aghalabu kwenye masuala ya kisheria. Uchunguzi huo hufanyika kwenye viambajengo vya lugha ambavyo upekee wake unajibainisha kwa mtu yeyote anayetumia lugha ya mazungumzo au maandishi.

Vilevile, tunapoitazama fasihi kama tawi la sanaa linalotumia lugha katika kufikisha ujumbe wake kwa jamii iliyokusudiwa, maana na matumizi ya lugha hujipambanua katika fani na maudhui. Mtunzi au Msanii wa kazi ya fasihi huweza kuelezea mawazo yake katika msuko wa matukio wenye kutumia viambajengo vya lugha ambavyo hufafanua visa vinavyoijenga kazi ya sanaa. Matumizi ya lugha katika fasihi hujitokeza kwenye mazungumzo na maandishi ambapo ndipo

tunapata fasihi simulizi na fasihi andishi. Fasihi andishi inajengwa na tanzu kuu tatu ambazo ni ushairi, riwaya na tamthiliya.

Kuhusu Uforensiki katika fasihi, Bondergaard (2017) amejadili jinsi kazi ya fasihi inaweza kuwa ya uforensiki. Kwa mantiki hii, kazi za fasihi zenye uforensiki zinaeleza kumbukumbu za matukio ya kihalifu na kuonesha namna ya kutambua umuhimu wa wahanga. Akitofautisha uforensiki katika kazi ya fasihi na ule wa mahakamani, Bondergoard (2017:5) anasema kuwa

> "*When the interpretation or presentation of evidence takes place in a literary work rather than in the courtroom, the evidence is, of course, interpreted according to a different logic. In the courtroom, forensics—as the art of the forum—tries to establish the facts about the event(s) in question and present them to the forum, potentially leading to conviction (or acquittal). In a forum surrounding a work of art the more general meanings raised by the particulars of the representation are exercised by the reader (see, for instance, Walsh 2007, 50).*
>
> Uwasilishaji wa ushahidi unapotolewa katika kazi za kifasihi badala ya mahakamani, ushahidi huo hufasiriwa kulingana na mantiki tofauti tofauti. Katika mahakama, uforensiki kama kiini cha sanaa jukwaani hujaribu kubaini ukweli kuhusu tukio au matukio husika na kuyawasilisha jukwaani ili kutoa hukumu au kuachwa huru. Maana ya jumla ya kazi ya sanaa inayowasilishwa jukwaani ndio inayozingatiwa na msomaji (Walsh, 2007:50). (Tasfsiri yetu)

Wataalamu wa fasihi na wahakiki wa kazi za fasihi, kwa muda mrefu, wamefanya tafiti kuhusu riwaya ya Kiswahili, hususani riwaya zenye matukio ya kihalifu, upelelezi na ujasusi na kuziona kuwa ni riwaya za kipelelezi au za mkondo wa kihalifu. Mlacha (1989, Madumula (2009) na Senkoro (1987) ni miongoni mwa wana taaluma waliotafiti na kuihakiki riwaya ya Kiswahili hususan riwaya zenye matukio ya kijasusi, ujambazi na mauaji kuziona kuwa ni riwaya za kipelelezi. Makala haya yanalenga kupanua mawanda ya uhakiki wa riwaya ya Kiswahili kwa kuichunguza riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale* ili kuonesha uforensiki unavyojitokeza na upelelezi, ukiwa ni miongoni mwa vipengele vya mbinu za kiforensiki. Aidha, yanaibua mtazamo mpya wa riwaya ya Kiswahili na uforensiki**.**

## Dhana ya Riwaya

Senkoro (1982) anafasili riwaya kuwa ni hadithi ndefu ya kubuni yenye visa vingi, wahusika zaidi ya mmoja na yenye mazungumzo yanayozingatia kwa undani na upana maisha ya jamii. Anaendelea kwa kusema kuwa riwaya inatoa picha yote ya ujumla wa maisha ya mtu toka nyumbani hadi katika kiwango cha taifa na hata dunia nzima.

Mlacha na Madumulla (1991) wanafasili riwaya kuwa ni hadithi iliyotungwa ambayo ina urefu wa kutosha, visa vinavyooana na kando na kuzingatia suala la muda. Kuhusu ukubwa, riwaya inaweza kuwa na kurasa zozote zile kwani si idadi ya maneno au kurasa tu ambavyo vitafanya tuviite hadithi fulani kuwa ni riwaya na nyingine kuwa ni hadithi fupi. Msokile (1992) anadai kuwa riwaya ni kazi ya sanaa ya kubuni na vileile ni maandishi ya nathari yanayosimulia hadithi ambayo kawaida ina uzito, upana, urefu wa kutosha. Madumulla (2009) anaeleza kuwa riwaya ni masimulizi marefu yakubuni yaliyo katika mtindo wa nathari, yakisawiri maisha ya mtu wa wakati maalum, mahali maalum na kwa madhumuni maalum. Mtu huyo anasawiriwa akiwa anawasiliana na nafsi yake, mwenzake au jamii yake.

Kwa jumla, tunaweza kusema kuwa riwaya ni masimulizi marefu ya kubuni yaliyo katika maandishi yanayoisawiri jamii husika. Stevick (1967) anauelezea utanzu wa riwaya kuwa umetanguliwa na maandiko marefu matatu ambayo ni tendi, romansi na tawasifu. Katika Bara la Asia, tunaona maandiko na historia ya riwaya hayajitokezi kwa wingi ila ni maandiko machache ambayo yalionesha masimulizi ya kiriwaya ambayo yalikuwapo tangu zamani kidogo. Huko India, katika karne ya saba, Dandin aliandika kitabu chake cha *Dasakumarakarita* kilichohusu masaibu ya wana kumi wa mfalme. Hii inatuonesha tuu kuwa masimulizi ya habari na historia mbalimbali za kale ndizo zilizo leta riwaya baada ya ujio wa maandishi.

Katika bara la Afrika, tunaona riwaya ilianza kujitokeza mwishoni mwa Karne ya 19 ikiwa imeletwa na elimu ya kimagharibi ilikuja na wakoloni. Maandiko ya kifasihi yalianza kujitokeza hapa na pale kama vile Afrika Kusini na Afrika magharibi. Walitokea waandishi walioandika hadithi za jamii zao kama vile Daniel Olorunfemi na Thomas Mofolo ambao waliandika hadithi za kizulu. Tunaona kuwa waliandika kwa lugha zao za asili na baadaye kazi zao zilitafsiriwa katika lugha zingine. Kuimarika kwa elimu kulisababisha kujitokeza kwa wasomi na waandishi wengine kama vile Amos Tutuola, Chinua Achebe, na wengine wengi wa huko Afrika magharibi na kati.

Kuhusu Afrika Mashariki, kazi za kinathari zilikuwa katika lugha za asili za jamii tofautitofauti kama vile Uganda na andiko la *Entalo za Buganda* (1894) kilichoandikwa na Apolo Kagwa akimaanisha vita vya Buganda. Pia, Okot p`Bitek aliandika kitabu chake kwa lugha ya Ki-luo, *Laktar kinyero wi lobo* akimaanisha una *meno meupe hebu cheka* (1953). Baadaye kazi za uandishi ziliongezeka na waandishi nao waliongezeka kama akina Taban loliyong, Okello Oculi, Robert Serumaga na wengineo.

Kuhusu Kenya, maandiko ya kinathari yaliandikwa kwa lugha za kimakabila kama vile Kikamba ambapo kuna kitabu cha *Mutunga na Ngewa Yake* (1954), yaani, Mutunga na hadithi yake kilichoandikwa na John Mbiti. Baadaye,

waliibuka waandishi, wasomi na wabobevu zaidi katika nathari za kubuni, lakini wengi wao waliandika kwa lugha ya Kiingereza, kwa mfano Mugo Gicaru, Josiah Mwangi Kariuki, Mugo Gatheru, James Ngugi (aliyebadili jina na kujiita Ngugi wa Thiong'o) ambaye aliamua kuachana na uandishi wa Kiingereza kwani ujumbeulioniwa hauifikii jamii aliyoikusudia. Hivyo, akaamua kuanza kuandika kwa lugha ya Kiswahili. Tunaona nathari ya ubunifu kwa Kiswahili zikatokea na waandishi wengi walioandika kwa Kiswahili waliongezeka, kwa mfano Katama Mkangi, Chacha Nyaigoti Chacha, Ngugi wa Miri na Kyallo Wadi Wamitila.

Kule Tanzania, riwaya za mwanzo kabisa zilizo katika Kiswahili ni *Habari za Wakilindi* (1885-1907) kilichoandikwa na A. H. L'Ajjemi, *Tulivyoona* na *Tulivyofanya Uingereza* cha H. M. T. Kayamba, *Mwaka Katika Minyororo* (1934) kilichoandikwa na M. Sehoza na *Uhuru wa Watumwa* (1934) cha James Mbotela, Shaaban Robert na Mohamed Said Abulla walionekana kuwa watunzi pekee wa kazi za kinathari zenye mvuto.

Madumulla (2009) anafafanua riwaya kama utanzu wa hivi karibuni ukilinganisha na ushairi na tamthilia. Ushairi ukimithilishwa na wimbo na tamthilia ikimithilishwa na uigizaji au utendaji ni fani ambazo zinakuwa na umri karibu sawa na historia ya mwanadamu. Anaendelea kueleza kuwa riwaya ilipata umbo ililonalo hivi sasa katika karne ya 18 huko Ulaya, na ikisadikiwa kuwa *Cyropaedeia* ndiyo riwaya ya kwanza kuandikwa na myunani Xenophon (430-355kk). Katika kipindi cha mwamko wa Sanaa (*renaissance*) huko Ulaya, kulitokea ongezeko la hamu ya utafiti na ugunduzi wa kisayansi na kiteknolojia ulioambatana na juhudi za kutalii na kuufahamu ulimwengu na malimwengu katika kuvumbua nchi mpya na njia iliofanywa na akina *Vespucci* na *Christopher Columbus*. Pia, tunaona katika ubepari wa viwanda ambao ulileta mapinduzi makubwa katika historia ya uandishi wa kazi za kubuni za kinathari. Kwa mara ya kwanza katika historia ya riwaya utaratibu wa kusawiri kwa kina maisha ya jamii katika uhalisi wake kwa kutumia lugha ya kila siku na mazingira yaliyozoeleka uliimarishwa.

**Riwaya ya Kiswahili**

Madumulla (2009) anafasili riwaya ya Kiswahili kuwa ni riwaya ambayo inalenga kumsawiri mtu na maisha yake katika kiwango cha taifa na si kiwango finyu cha jamii fulani ndogo. Anaendelea kusema kuwa kuna riwaya ya Kiswahili ambayo inalenga kujenga na kuaridhia mila, desturi, jadi na utamaduni wa mtu katika ngazi ya taifa na kasi hiyo inazidishwa na utandawazi ambao tayari unaelekea kutuvusha hata kwenye mipaka ya kitaifa. Samweli (2015) anasema kuwa riwaya ya Kiswahili ni nathari iliyoandikwa kwa Kiswahili. Katika makala haya, tunaweza kusema kuwa riwaya ya Kiswahili ni riwaya iliyoandikwa kwa Kiswahili huku ikisawiri tajiriba ya maisha na mazingira ya jamii husika.

Madumulla (2009) anaielezea historia ya riwaya ya Kiswahili tangu kipindi cha ujio wa Wamishenari ambao walikuja na teknolojia ya uandishi. Nathari tangulizi inayojulikana kuandikwa na mwenyeji ni *Habari za Mrima* iliyoandikwa na Sheikh Ali bin Hamed (1880) ijapokuwa ilichapishwa 1935 katika jarida la Kiswahili la *Mambo Leo*. Nathari nyingine ni *Habari za Wakilindi* iliyoandikwa na Abdallah bin Hemed bin Ali el Ajjemy ambaye ni mzaliwa wa Zanzibar kwa baba wa kiarabu na mama wa kihehe. Maandiko haya yaliandikwa katika kipindi cha wajerumani.

Katika kipindi cha Waingereza, tunaona msisitizo ulikuwa ni kwenye elimu ya darasani na juhudi ilikuwa ni namna ya kuvipata vitabu kwa kuandika na kufanya tafsiri. Kwa mfano, vitabu vilivyofanyiwa tafsiri ni hadithi *za Esopo, Safari ya Msafiri, kisiwa chenye Hazina, safari ya Allan Quartermain na Wenzake* na *Mashimo ya Mfalme Suleiman, Alfu Lela-u-Lela.* Tunaona maandiko haya yalitumika sana hadi kufikia miaka ya 1950 ndipo ambapo waandishi wenyeji walijitokeza kwa wingi na kuandika nathari bunilizi za Kiswahili kwa kufuata mikondo kama: mkondo wa kisafari na kimaadili ambao tunaona nathari ya kubuni kwa Kiswahili ni *Uhuru wa Watumwa* (1934) iliyoandikwa na Jamaes Mbotela, *Kusadikika* (1951) na *Kufikirika* (1952) zilizoandikwa na Shaaban Robert. Mkondo mwingine ni wa kinyaraka ambao ulikuwa na nathari bunilizi kama vile *Bwana Myombekere na Bibi Bugonoka* iliyoandikwa na Anicet Kitereza na kuchapishwa 1981, *Kurwa na Doto* (1951) iliyoandikwa na Saleh Farsy, *Mzishi wa Baba Ana Radhi* iliyoandikwa na Felician Nkwera. Mkondo mwingine ni wa kihalifu na kipelelezi. Mkondo huu ulifunguliwa na riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale* (1957) iliyoandikwa na Mohamed Said Abdulla ikiwa ni matokeo ya mashindano ya uandishi wa hadithi za kubuni kwa Kiswahili ambayo yaliandaliwa na kamati ya Lugha ya Kiswahili Afrika Mashariki. Mohamed Said Abdulla ameandika vitabu vingine kama vile *Kisima cha Giningi* (1968), *Duniani kuna Watu* (1973) *Mwana wa Yungi Hulewa* (1976), *Kosa la Bwana Msa (*1984). Pia, waandishi wengine wa mkondo huu ni Faraji katalambula aliyeandika riwaya ya *Simu ya Kifo* (1966), mwingine ni Aristablus Elvis Musiba aliyeandika riwaya za Kikosi cha Kisasi (1979), *Kufa na Kupona* (1974), *Njama* (1978), *Kikomo* (1980), na *Hofu* (1987).

Mkondo mwingine ni wa kijamaa ambao uliibuka katika kipindi cha Azimio la Arusha, kwa mfano: riwaya kama vile *Njozi za Usiku* (1972) iliyoandikwa na W. Seme, *Ndoto ya Ndaria* (1975) iliyoandikwa na J. Ngomoi, *Shida* (1975) iliyoandikwa na Ndyanalo Balisidya, *Kuli* (1974) iliyoandikwa na Shafi Adam Shafi, *Dunia Uwanja wa Fujo* (1980) iliyoandikwa na Said Mohamed. Mkondo mwingine ni wa uhalisia teti, yaani, kihakiki ambao ulikuwa ukihoji juu ya azimio la Arusha na makubalianao yaliyowekwa kutekelezwa, ambapo riwaya kama vile *Nyota ya Huzuni* (1978) iliyoandikwa na G.Liwenga na *Njozi liyopotea* (1979) iliyoandikwa na C. Mung’ong’o, *Kichwa maj*i (1974) na *Gamba la Nyoka* (1978)

zilizoandikwa na E. Kezilahabi, *Sudi ya Yohana* (1981), *Almasi za Bandia* (1991), *Makuwadi wa Soko Huria* (2002), *Kivuli* zilizoandikwa na C. L. S. Chachage, *Vuta N'kuvute* (1999) iliyoandikwa na Shafi Adam Shafi. Mkondo mwingine ni wa kifatakari au falsafa ambao ulijikita katika kuyatafakari maisha na mazingira yake. Mfano wa riwaya za mkondo huu ni *Rosa Mistika* (1971), *Dunia Uwanja wa Fujo* (1976), *Nagona* (1987), *Mzingile* (1990) zilizoandikwa na Euphrase Kezilahabi, *Ziraili na Zirani* (1999) iliyoandikwa na William Mkufya, *Babu Alipofufuka* (2001) iliyoandikwa na Said Ahmed Mohamed, *Shetani Msalabani* (1982) iliyoandikwa na Ngugi wa Thiong'o. Pia, upo mkondo wa ufungwa ambao ulijikita katika kuyasawiri mazingira ya gerezani na masuala ya magereza. Mfano wa riwaya za mkondo huu ni *Umleavyo* (1990) iliyoandikwa na Maulid Haj, *Siku ya Watenzi Wote* (1968) iliyoandikwa na Shaaban Robert.

Samweli (2015) anaielezea riwaya ya Kiswahili katika vipindi vinne ambavyo ni riwaya ya Kiswahili kabla ya karne ya 19 ambapo anaona kuwa kabla ya ujio wa wakoloni, hakukuwa na riwaya yoyote ila masimulizi ya kinathari yaliyohusiana na ushairi. Maandishi haya yalikuwepo kwa lugha ya Kiarabu: *Siri 'lAsirari* kililchoandikwa na Binti Lemba (1966), *Masimulizi ya Wakilindi* iliyoandikwa na Abdalla bin Hemed bin Ali el Hamed yaliyochapishwa katika majuzuu matatu ambayo ni 1895, 1904, 1905. Masimulizi mengine ni *Maisha ya Hamed bin Muhammed el Murjebi* au *Tippu Tip* (1902) iliyoandikwa na Hamed bin Muhammed el Murjebi. Kipindi kingine kinaendana na majilio ya ukoloni. Katika kipindi hiki, tunapata watafsiri wa kazi nyingi za fasihi iliyoenezwa miongoni mwa waswahili. Mfano ni *Safari za Msafiri* (1925), *Mashimo ya Mfalme Suleiman* (1929), *Kisiwa chenye Hazina* (1929), *Jamaa hodari Kisiwani* (1951) *Robinson Kruso na Kisiwa Chake* (1962). Pia, walianzisha shule ambazo zilikuza waandishi wengi wa Kiswahili kama vile James Mbotela aliyeandika riwaya ya *Uhuru wa Watumwa* (1934), Shaaban Robert aliyeandika *Kusadikika* (1951) *Kufikirika* (1947), *Adili na Nduguze* (1952).

Katika kipindi cha uhuru, riwaya ya Kiswahili inajielekeza katika kuufurahia uhuru. Mfano wa riwaya zilizoandikwa katika kipindi hiki ni *Utu bora Mkulima* (1968), *Siku ya Watenzi wote* (1960), *Gamba la Nyoka* (1979), *Njozi iliyopotea* (1980) na zinginezo za mrengo huo. Kipindi cha Utandawazi, riwaya zinazojitokeza ni zile za kiuhalisia, kiuhakiki pamoja na za kimajaribio na riwaya pendwa zilizoandikwa kwa wingi sana kwani zilionekana kuwa na soko. Riwaya pendwa ni zile zilizohusu masuala ya mapenzi, upelelezi, uhalifu na ujambazi.

Ifahamike kuwa ufafanuzi wa mikondo na vipindi vya historia ya riwaya ya Kiswahili haujafunga lango la uandishi katika kila mkondo au kipindi. Uandishi bado unaendelea kutokana na kwamba wimbi la waandishi kwa zama hizi za sayansi na teknolojia ni jingi na kila mmoja huweza kuchunguza historia ya maisha halisi na kubuni kuandika riwaya katika mkondo au kipindi chochote akipendacho kati ya hivyo tulivyovitazama.

**Nadharia ya Mwingiliano Matini**

Makala haya yanatumia nadharia ya mwingiliano matini hasa kutokana na sababu kwamba uchambuzi unahusu taaluma ya uforensiki inavyotagusana na fasihi kupitia riwaya ya Kiswahili. Kupitia misingi ya nadharia muingiliano matini, makala yanakusudia kubainisha mtagusano uliopo wa uforensiki katika riwaya ya Kiswahili. Graham Allen (2000) anaifafanua nadharia ya muingiliano matini kama yenye chimbuko lake katika nadharia ya Umuundo. Kuanzishwa kwa nadharia ya muingiliano matini kulitokana na mabadiliko ya kisiasa nchini Ufaransa ambayo yalizua mjadala na kuikosoa nadharia ya umuundo, hususan katika nafasi ya mwandishi katika kazi ya fasihi na maana. Mjadala ulijikita katika kuikosoa hoja isemayo kuwa mwandishi pekee ndiye anayejua maana ya kazi ya fasihi.

Adophe Heberer (2007) anaeleza kuwa istilahi muingiliano matini ilianza kutumiwa katika maandishi na Julia Kristeva katika makala ya Bakhitin. Ingawa ilikuwepo kabla, ilikuwa ikihusishwa na dhana fulani ambazo zinaonekana kufanana na muingiliano matini. Wananadharia wa usasa kama vile T. S. Eliot, Gerard Genette na Umberto Eco wameielezea nadharia ya muingiliano matini inavyojitokeza katika kazi za fasihi kutokana na kazi za fasihi kujenga maudhui na fani yake kutokana na maisha ya wanajamii husika.

Graham Allen (2000) anaeleza zaidi kuwa muingiliano matini haujafungwa kwenye kazi za fasihi tu, bali unahusisha pia kazi, au taaluma zingine zisizo za kifasihi. Anaeleza sifa muhimu za muingiliano matini hukosa upekee, kwani matini moja hutegemea kuwepo kwa nyingine. Uwezo wa msomaji kuvunja huo upekee kwa kujenga mahusiano na zingine kwa kuoneza mawazo, huupa nguvu mtazamo wa Barthes unaohusu msomaji kutoa maana ya kazi.

Msingi wa nadharia ya muingiliano matini ni kuwa kila kinachotokea katika kazi mpya ni kitu kilichotokea kila mara katika kazi tangulizi. Umberto Eco anaeleza kuwa kazi yoyote hujengwa na kazi na kuwa matini hujengwa na matini na, kwa pamoja, husemezana bila kutegemea lengo la mwandishi. Kutokana na hoja hii, kazi ya fasihi ni zao la kazi nyingine zilizo na zisizo za kifasihi. Mambo yanayoakisi muingiliano matini ni pamoja na wahusika, muktadha, matumizi ya taswira, unukuzi, muundo na maudhui.

Pia, nadharia ya muingiliano matini inatusaidia kuielewa riwaya ya Kiswahili namna ilivyobuniwa na hata katika uchunguzi wa uforensiki unavyojitokeza katika riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale.* Tunaweza kusema kuwa upokezi na uelewaji wa utanzu kama riwaya unategemea kuwako kwa riwaya au matini fulani kabla ya riwaya maalum inayochunguzwa. Ikumbukwe kuwa nadharia ya muingiliano matini si nadharia ya uchunguzi wa vyanzo au athari za kazi fulani, ila huhusisha mitindo fulani ya ki-usemi na misimbo fulani ambayo imesaidia katika uashiriaji wa kazi za fasihi zijazo. Wamitila (2000) anaeleza kuwa maana

ya matini inaangaliwa kama inayotegemea matini nyingine na kuwa matini yoyote hufaidi kutokana na matini fulani. Nadharia ya muingiliano matini inatupa uwanja mpana kutumia matini mbalimbali zihusuzo uforensiki katika kuelezea uforensiki kwenye riwaya ya Kiswahili hususan riwaya teule. Aidha, inaweza kutumika katika kuchambua kazi za kifasihi na zisizo za kifasihi.

## Nadharia ya Muingiliano Matini katika Kuchunguza Mtagusano wa Uforensiki katika Mzimu *wa Watu wa Kale* na *Kosa la Bwana Msa*

Kama tulivyotoa maana na dhana nzima ya mtagusano kuwa ni muingiliano wa vitu viwili au zaidi katika kuleta ukamilishano.Uforensiki ni taaluma pana ambayo inatumia mbinu za kisayansi na teknolojia katika uchunguzi na upelelezi wa masuala yenye utata kwenye jamii husika, aghalabu masuala ya kihalifu na utoaji wa hukumu. Kwa muda mrefu sasa, taaluma hii ya uforensiki imejitokeza sana kwenye nyanja za sayansi na sheria. Malcolm (2017) anaeleza kuwa hivi karibuni, uforensiki umeanza kujitokeza kwenye sarufi ya lugha katika kutambua, kubainisha, kuainisha na kutathmini uhalisi wa jambo kwa kutumia mbinu za kisayansi na teknolojia ili kupata ushahidi thabiti kuhusu jambo fulani katika jamii.

Skinner (2014) anaeleza namna uforensiki unajitokeza katika riwaya za Shakespeare akirejelea riwaya ya “*Mechants of Venice*”, anaonesha jinsi mbinu za matumizi ya lugha kama vile balagha katika majukwaa ya kisheria, usimulizi wa ushahidi wa kiutamaduni wa Uingereza unaojipambanua kama visasili, matumizi ya msamiati katika kujenga hoja zinazopingana na uhalisi wa jambo. Kutokana na uchambuzi wa Skinner katika kuelezea uforensiki unaojitokeza kwenye riwaya za Shakespeare kama riwaya ya *Mechants of Venice* ambayo ilitafsiriwa na Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na kujulikana kwa jina la Mabepari wa Venisi, inatupa ithabiti kuwa uforensiki unaweza kujitokeza katika riwaya zingine hususan riwaya ya Kiswahili.

Malcolm na wenzake (2017) wanaeleza kuwa uforensiki katika fasihi unajitokeza katika mtindo wa usimulizi wenye ushahidi wa kiujumi utokanao na uchunguzi wa mambo ya kale. Zaidi, wanaeleza namna uforensiki unaweza kujipambanua kwenye msuko wa matukio, matumizi ya lugha, usimulizi na matumizi ya midia za kuona.

## Mtagusano wa Uforensiki katika riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale*

Uchunguzi wa uforensiki katika riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale* na *Kosa la Bwana Msa* unajitokeza katika vipengele vingi. Makala haya yanachambua vipengele vikuu vitano ambavyo ni Muktadha, Msuko wa matukio, Matumizi ya Lugha, wahusika na Mgogoro. Kupitia vipengele hivyo, tunaweza kuudhihirisha mtagusano wa uforensiki katika riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale.*

**Muktadha**

Kimsingi, muktadha ni kipengele muhimu katika kazi yoyote ya kifasihi, na hujumuisha mahali na wakati kazi hiyo ya kifasihi imetendeka. Katika taaluma ya uforensiki kwenye mchakato wa uchunguzi wa tukio namna lilivyotendeka, mazingira ya tukio ni muhimu katika kusaidia upatikanaji wa vithibiti kama vile, udongo, vifaa vyovyote vilivyoachwa, eneo la tukio, mwili wa marehemu aliyefanyiwa uhalifu ambaye atafanyiwa uchunguzi kwa kuangalia alama za vidole, damu, nywele, macho n.k.

Katika riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale*, tunaona eneo la mzimuni ambako kuna mwili wa Bwana Ali uliokatwa kichwa. Katika harakati za kumtafuta Bwana Ali, Bwana Msa na Najum wanamkuta katika kichaka cha mzimu wa watu wa kale. Bwana Msa anasema "njoo Najum umtazame Bwana Ali kakatwa kichwa" (uk 35). Pia suala la wakati ambao Bwana Ali alipita Mzimuni linajitokeza. Tunaona alipita wakati wa usiku tena peke yake na hili linajidhihirisha pale ambapo Inspekta Seif alimhoji Banyani kwa kusema.

> "sikiliza Seti, mimi ma makuja nataka uliza we'kidogo. Jana wakati wa magharibi Bwana Ali, jirani yako ameonekana makuja hapa kwako. Hebu eleza kidogo, Bwana Ali makuja hapa fanya nini" (uk 62).

Katika muktadha huu, tunaona muda ambao Bwana Ali aliondoka, sambamba na tukio la kukatwa kichwa vinatujengea taswaira ya uhalali wa kutendewa tukio la kinyama na mtu au watu. Taarifa hizo zinahitaji ufafanuzi wa kina ili kujua chanzo na mhusika.

Aidha, muktadha mwingine unaodhihirisha uforensiki ni pale ambapo Inspekta Seif wakati alipokuwa akipeleleza mauaji ya bwana Ali, alimwuliza maswali Mmanga, kwani tukio la mauaji lilitokea karibu na mazingira ya nyumba yake. Alipomwuliza mgeni wake yuko wapi, Mmanga alimjibu kuwa hakujua alipo, na kwamba alichojua ni mgeni aliyetokea Maskati mwenye asili ya Kongo na amekuja huku Uswahilini. Tunaona kutoonekana kwa mgeni huyo kulimpa maswali Inspekta Seif na kuamua kumsaka ili kupata ukweli halisi kuhusu aliyehusika na tukio hilo la mauaji (uk55-58).

**Msuko wa Matukio**

Katika riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale*, tunaambiwa Bwana Msa alimwona Bwana Ali katika makaburi ndani ya kichaka cha mzimu wa watu wa kale. Kisha akamwita Najum, "mtazame Bwana Ali kakatwa kichwa" Najum akazidiwa na hofu kwani yule aliyekuwa amekaa pale chini ya kaburi, hali amenyoosha miguu yake na kupakata kichwa chake, alikuwa Bwana Ali" (uk35). Jambo tunaloliona hapo ni tukio ambalo linatoa ushahidi kamilifu kuhusu kifo cha Bwana Ali. Kinachobaki ni kuanza kufanya uchunguzi juu ya mtu aliyesababisha mauaji ya Bwana Ali. Uchunguzi ulihusisha chombo cha dola, yaani polisi, ambapo Inspekta Seif na Najum waliokuwa wanahaha kutafuta aliyetekelza mauaji.

Tukio lingine linalojenga taharuki ni pale Inspekta Sefu na Bwana Musa walipokwenda nyumbani kwa Babiani na kuanza kumuhoji na alipoingiwa na hofu yeye na Boi wake. Ni jambo linaloonesha kanakwamba wao ndio wamehusika na mauaji hayo (59-65). Bila uchunguzi wa kina tunaweza kusema kuwa Baniani na Boi ndio waliomuua Bwana Ali.

Hapo tunaona namna mtunzi alivyopangilia msuko wa matukio yenye kuleta taharuki ya kutaka kujua zaidi na katika uforensiki ni muhimu kujua namna tukio lilivyotokea na kutokana na mfululizo uliopo unaouleta tafakuri ya kina na kuunda maana akilini mwa mtu inayohitaji uthibitisho wa kiforensiki na siyo kuhisi tu.

**Mgogoro**

Mgogoro ni mvutano baina ya pande mbili au zaidi, mtu na mtu, kundi au hata mtu na nafsi yake. Katika kazi yoyote ya kifasihi, migogoro huweza kujitokeza ikiwa na lengo la kukuza kisa ambacho kwacho mtunzi anakisimulia na kuonesha chanzo cha matukio yatakayoendelea katika kisa hicho na pengine hata kudokeza mchakato wa suluhisho linalotarajiwa. Katika taaluma ya uforensiki, mgogoro hutumika kama kiini cha tatizo ambacho ni muhimu kukichunguza ili kupata ukweli wa matukio yaliyotendeka, hususan, yaliyosababisha mauaji.

Katika riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale*, tunaona mgogoro unaanza kujitokeza pale ambapo Bwana Ali haonekani nyumbani kwake na jitihada za kumtafuta zinaanza. Baada ya uchunguzi kufanyika, tunaona inajulikana kuwa mwili wake umepatikana katika kichaka cha mzimu wa watu wa kale. Tunaona mgogoro mwingine unazuka wa kusaka chanzo cha kifo chake na kudhania kuwepo kwa mvutano kati ya Baniani na Bwana Ali baada ya Bwana Ali kumuuzia Banyani mali yake yote na akapewa elfu hamsini na akabakisha elfu kumi ambayo alitakiwa kupokea baadaye. Kisaha, Baniani anatoa maelezo hayo kwa Bwana Msa na Najum. Walijaribu kumdodosa kwa lengo la kupata ukweli kuhusu kifo chake.

Bwana Msa na Inspekta Seif wanapokea maelezo kutoka kwa Baniani. Maelezo hayo waliyoyapata kwa uchunguzi wa saikolojia ya kiforensiki wanamuona ni dhaifu hawezi kumuua Bwana Ali kwa pigo moja la panga. Mgogoro mwingine unaoleta tafakuri katika kuchunguza kifo cha Bwana Ali ni kati ya Bwana Ali na Mwarabu ambaye alidai kuwa alimuharibia nyumba yake walipokuwa Kongo kwani alikuwa na pesa nyingi za kufisidia wake za watu (uk 75-76). Mgogoro huo ulijenga uhasama uliodumu muda mrefu. Mwarabu alikuwa na kinyongo na Bwana Ali ambacho kilitatuliwa na yeye kulipiza kisasi kwa kumuua Bwana Ali bila ya kujali kuwa hatima yake. Ushahidi unaonekana wazi kutokana na Bwana Msa kuwa na maelezo yote kuhusiana na watu hao wawili na kisa chao walipokuwa wanaishi Kongo. Ushahidi huo unajitokeza pale ambapo Mwarabu alikamatwa akitaka kutoroka kwa jahazi; alikiri kumuua Bwana Ali.

Hapa, inathibitika kuwa Bwana Ali aliuawa na yule Mwarabu mgeni (uk 66) kwani alikiri kuwa yeye ndiye alimwua Bwana Ali (uk 75-76).

> "…Bwana Ali alimwona mtu Mwarabu mkubwa wa kimo, mkubwa wa umbo, anakuja huku kutoka Bareste, kachukua upanga; naye aliweza kumtambua kuwa ni Yule mgeni wa Mmanga wa Bareste aliyekuja kutoka Maskati juzijuzi. Bwana Yule alikuwa kweli ameazimia shari na ubaya juu ya Bwana Ali… Alipomwona tu alifuta upanga wake akamfuata mbio. Bwana Ali hakuwahi kukimbia hata hatua sita mara alimfikia, akakirusha kichwa chake kwa upanga" (uk 65-66).

Mgogoro mmojawapo umeleta suluhisho la kifo cha Bwana Ali. Hii ni mbinu ya msingi katika taaluma ya Uforensiki ambayo inadadisi kuchunguza mivutano inayohisiwa kuwa chanzo cha uhasama na kusababisha visasi vya mauaji. Vilevile, katika fasihi, migogoro hutumika katika kujenga visa vya matukio vinavyoonesha mchakato wa kisa kizima cha hadithi. Mwingiliano huu unaojitokeza katika migogoro na hata vipengele vingine unathibitisha uwepo wa taaluma mbili, yaani, fasihi na uforensiki katika utungaji wa riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale.*

**Matumizi ya Lugha**

Katika kazi ya fasihi, matumizi ya lugha yanajipambanua kwenye vipengele tofauti tofauti kama vile tamathali za semi, methali, nahau, vitendawili na vilevile lugha ya picha na taswira na kadhalika. Katika riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale*, matumizi ya lugha yanajitokeza pale kwenye kitabu cha Bwana Msa kilichoitwa *Kinyume cha Mambo* ambacho alikitumia Bwana Msa katika kuhifadhi kumbukumbu za mambo mbalimbali. Wengi walishindwa kukielewa kitabu chake kwani alitumia mtindo wa uandishi aliouelewa yeye mwenyewe (uk 8-13).

Vilevile, matumizi ya kitendawili ambapo Bwana Msa anamwambia Najum kuwa Mtu akikwambia 'popombili za vuka mto' sharti utie akilini kwako kuwa popoo ni kitu dhaifu sana na kuwa udhaifu wake huzitaraji kuwa zitaweza kuvuka mto maji yanapopita kwa kasi (uk30-31). Matumizi ya lugha ya kingereza yametukika pale ambapo Najum alimwita Bwana Msa kuwa ni Sherlock Holmes na Bwana Msa akapokea kusifiwa huko kwa kuzungumza lugha ya kiingereza akisema "Simple, my dear Watson, quite simple. You know my methods" (uk 40-41).

Matumizi ya maswali ya kidadisi yenye kumtisha muulizwaji yamejitokeza kwa Insekta Sefu alipomuuliza Mmanga maswali bila ya kupepesa macho huku akimtazama usoni na kusema "mgeni wako yuko wapi? Na anatoka Maskati, siyo? Na upanga wako uko wapi? (uk 52-55). Tunaona ni maswali yaliyomwogopesha muulizwa na yalifanya utafiti uwe rahisi kwani kila

aliyeulizwa alijibu kwa hofu huku akitoa taarifa zote alozozijua juu ya kile alichoulizwa.

**Wahusika**

Katika sehemu hii tunawatazama kama ni binadamu au viumbe wasio binadamu kuvalishwa uwezo wa binadamu katika utendaji ambao ndio hutumika kutenda matendo mbalimbali yanayoijenga kisa katika kazi ya fasihi. Katika riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale*, mwandishi ametumia wahusika binadamu kama vile Bwana Msa, Bwana Ali, Najum, Kipwerere, Inspekta Seif, Mwarabu, Baniani ambao tunaona kila mmoja amebeba uhalisia wa tabia za watu ambao wapo kwenye jamii. Kwa mfano, Inspeka Seif anajitokeza kama askari mpelelezi wa masuala ya jinai. Jinsi alivyohusika katika kupeleleza mauaji ya Bwana Ali hata kumkamata Mwarabu kuwa ndiye muhusika wa tendo hilo la kikatili, ni Ushahidi mwafaka na weledi wake katika taaluma hii.

Pia Bwana Msa amejitokeza kuwa mtu mwenye uelewa wa juu na hekima ambazo zilimwezesha kuhifadhi kumbukumbu za habari na matukio mbalimbali katika kitabu cha *Kinyume cha Mambo* ambacho ni yeye pekee aliyekielewa. Kilimsaidia hata wakati wa kumtafuta Bwana Ali na kujua nani alihusika na mauaji yake. Alikumbuka jinsi alivyowahi kusimuliwa kuhusu mgogoro wa Bwana Ali na Mwarabu tangu akiwa Kongo. Kumbukumbu ya simulizi hiyo ilimwezesha kujumuika katika uchunguzi wa kina kuhusu mauaji hayo na hatimaye walifanikiwa kubaini utata huo.

Kwa jumla, wahusika wengine wengi waliotumiwa katika kujenga visa mbalimbali wanatambulisha tabia za watu ambao wapo kwenye jamii. Hili linatuonesha namna ambavyo utunzi wa kazi ya fasihi unategemea ujenzi wa wahusika wenye kubeba tabia za watu halisi waliopo katika jamii ili kufikisha ujumbe sahihi kwa jamii.

**Hitimisho**

Kutokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia yaliyopo sasa, fasihi inapaswa kupanua mawanda yake katika uhakiki na utafiti. Hii ni kutokana na maarifa na taaluma kuongezeka ambazo hutumia sayansi na teknolojia katika kurahisisha mchakato wa masuala mbalimbali yaliyopo katika jamii. Tunaona makala haya yameonesha mtagusano wa uforensiki na riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale* ambapo unathibitisha uwepo wa mwingiliano wa taaluma hizi mbili yaani fasihi na uforensiki kujitokeza katika riwaya kunaonesha na kuthibitisha lile dai la msingi wa nadharia ya mwingiliano matini lililowekewa msingi wake na Julia Kristeva katika makala ya Mikhail Bakhtin huko Ufaransa, kuwa hakuna matini inayoweza kuangaliwa kivyake au kipekee, pasina kuhusishwa na matini nyingine. Dai hili linashadadia hoja ya kuwa maana ya kazi ya fasihi hupatikana kwa kuhusianisha na matini zingine za kifasihi au zisizo za kifasihi. Kutokana na ufafanuzi uliotolewa katika makala haya kuhusu mtagusano wa uforensiki na

riwaya ya Mzimu wa Watu wa Kale kwa kuviangalia vipengele vya muktadha, msuko wa matukio, mgogoro, matumizi ya lugha na wahusika.

Hivi ni baadhi ya vipengele vichache kati ya vingi tulivyoweza kuvijadili ambavyo vinaoonesha mtagusano wa taaluma hizi mbili. Jambo ambalo tukilitazama kwa kina tunaona kuwa fasihi kama kilelezo cha kisanaa kitumiacho lugha kufikisha ujumbe wake kwa jamii iliyokusudiwa hutegemea ujenzi wa kazi yake kupitia matukio, wahusika, muktadha wa jamii unaojegwa na wahusika na mahusiano yao katika jamii husika. Hapo ndipo tunapoona riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale* ikiwa na simulizi iliyojengwa na taaluma ya uforensiki na fasihi.

Aidha, makala haya yanatoa wito kwa wanataaluma wengine kuanza kumakinikia taaluma ya uforensiki kwa kufanya tafiti katika uga wa fasihi ili kuendelea kuongeza marejeo katika riwaya ya Kiswahili kwenye zama hizi za sayansi na teknolojia na kuendelea kuifafanua kwa kina dhana ya uforensiki katika fasihi ya Kiswahili.

## Marejeleo

Abdulla, M. S. (1960). *Mzimu wa Watu wa Kale*. Nairobi na Dar es Salaam: East African Literature Bureau.

Bondergaard, H. (2017). *Forensic Memory: Literature after testimony*. Glasgow, UK: Univesity of Glasgow.

Madumulla, J. S. (2009). *Riwaya ya Kiswahili: Nadharia, Historia na Misingi ya Uchambuzi*. Dar es Salaam: Mture Education Publishers Ltd.

Malcolm, C. et. al. (2017) *Introduction to Forensic Linguistics: Language in Evidence*. London: Cenveo Publisher Services.

Mlacha, A. S. K. na Madumulla, J. S. (1993). *Riwaya ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Mlacha, S. A. K. (1984). *"Riwaya za Visiwani (1970-1980) na Ujenzi wa Jamii mpya" katika Mulika Namba 16*. Dar es Salaam: TUKI.

Samweli. M. (2015). *Umahiri katika Fasihi ya Kiswahili: Mwongozo kwa Wanafunzi na Walimu wa Fasihi Simulizi na Andishi*. Dar es Saalam: Mevel Publishers.

Senkoro, F. E. M. K. (1982). *Fasihi*. Dar es Salaam: Press and Publicity Ceneter.

Skinner, Q. (2014). *Forensic Shakespeare*. Oxford: OUP.

Wamitila, K. (2003). *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Books.